

Song 3 – Shida za Dunia

Artists: Jose Chameleone

Language Swahili

Video URL <http://www.youtube.com/watch?v=26ZrnTwwUfE>

Maana ya maneno (Words and Expressions Explained)

Fulani- certain

kufukuzwa kazini- expelled from work

kutoroka- run away from someone or something

amechoka- he is tired

kujuta- to regret

tulia- cool down

anakujaribia- he is testing you

usikonde- do not lose wait (literary meaning) , do not worry,

usijali- do not worry

maisha makali- tough life

Tizama- look

Kichekesho- laughter

Maisha yatakuwa na matatizo

Mungu – God

Kufikiri- think

Peke yako-by your self

Kupanga- to arrange, to plan

Kuambia- to tell

Acha kulia- stop crying shida za dunia

Hebu tulia Mungu anakujaribia

Masuali (Questions)

1. Rafiki yake alikuwa na shida gani?
2. Kitu gani kilitokea baadae?
3. Kitu gani kinamchosha?
4. Kwanini mwimbaji anamsihi rafiki yake kuwa asilie?
5. Jee ni rafiki wa mwimbaji tu ndie ambae ana shida?
6. Mwimbaji anampa ushauri gani rafiki yake anapokuwa na matatizo?
7. Kitu gani ambacho rafiki wa mwimbaji anajaribiwa?
8. Andika maelezo kwa ufupi uelezee hii nyimbo anazungumzia nini(inahusu nini)

Mazoezi (Exercise)

1. Sikiliza nyimbo kwa makini na andika maneno ambayo yanakosekana (Listen to the song carefully and find the missing words)

Verse 1

Rafiki yangu _____ nyumbani _____ shida fulani

Ati _____ kazini na _____ atafanya nini

Mke wake _____

Rafiki zake _____

_____ amepata nyingi _____

Dunia _____

Acha _____ shida za dunia

Hebu _____ Mungu _____

Verse 2

_____ mwendo ni pole

Ukipata shida leo _____

Wengi _____ kama wewe _____

Acha kulia ni maisha _____

_____ kwanza uone kesho

_____ uwape kichekesho

Maisha yatakuwa na _____

_____ Mungu atakupa _____

Verse 3

Hizo _____ usifikirie uko nazo peke _____

Labda Mungu anakuletea _____

_____ jua kama leo sio yako

Kwahiyo _____ usikonde

_____ kesho utapata

Mungu alipanga maisha kakaraka

Unapanga naye _____

Shida za dunia _____

Acha _____ shida za dunia

Hebu _____ Mungu _____

2. Andika kwa ufupi useme nyimbo hii inazungumzia nini?
3. Andika hadithi ya kuelezea kinachozungumzwa katika nyimbo hii.
4. Unafikiri kisa cha nyimbo hii kinaweza kutokea hapa Marekani?
Kwanini?Umewahi kukisikia kisa kama hiki au kinachofanana na hiki?
5. Jee ushauri alioutoa mwimbaji kwa rafiki yake unafikiri utamsaidia? Kwanini?
6. Andika sentensi zenye maana kwa kutumia maneno yafuatayo. Kila sentensi isipungue maneno 15:
 - i. kufukuzwa kazini
 - ii. kujuta
 - iii. Kichekesho
 - iv. Kufikiri
 - v. Peke yako/yangu/yao
 - vi. Kuambia
 - vii. Kuacha kulia